

»»Ufugaji wa Samaki aina ya sato ni biashara yenye faida kubwa inayotoa kipato kwa mamilioni ya watu duniani«

Kwa kuwa ni biashara nzuri, ubora na wingi wa samaki hutegemea kiwango na mbinu ya uzalishaji inayotumika.

Ufugaji wa samaki aina ya sato ni biashara yenye faida kubwa kutohana na ladha na lishe yake. Kwa ufugaji wa samaki aina ya sato, watolee chakula sahihi na maji safi kwani hii huongeza ukuaji na uzalishaji wa samaki.

Usimamizi wa samaki

Kwa usimamizi bora, fuga idadi sahihi ya samaki kwenye bwawa lako. Ikiwa unatumia bwawa kufuga samaki, ondoa maji yote na uliache kwa muda wa mwezi mmoja kabla ya kuanza upya kulitumia. Pia ondoa samaki wote kutoka kwa bwawa kwa kutumia wavu.

Safisha bwawa kwa kuondoa magugu yote pamoja na wanyama, na uliache likauke vizuri kwa wiki moja au zaidi. Weka samaki wachanga 20–25 kwa kila mita mraba kwenye mabwawa madogo. Jaza bwawa na maji safi mara moja kabla ya kuweka samaki wachanga.

Kwa ufugaji wa kibiashara, weka samaki 2–3 kwa kila mita mraba, na uwape chakula cha dukani na chakula cha kikaboni. Sato hukomaa baada ya siku 240 na huvunwa kwa kutumia wavu.

Hatimaye, uza samaki moja kwa moja sokoni au uza samaki waliosindikwa. Weka samaki kwenye makopo kwa ajili ya kuuza kwenye soko la nje.